

# SAUTI ZA WATANZANIA-CHUNGUZI KIFANI JUU YA BIASHARA NA HAKI ZA BINADAMU

# (TOLEO LA 2): "HAKI ZA ARDHI NA MAZINGIRA"

**Swahili summary**

## UTANGULIZI

Ardhi ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini Tanzania, na hasa kwa wale waishio katika mazingira ya vijijini[1]. Huko, upatikanaji wa ardhi na rasilimali za ardhi kunahusiana moja kwa moja na uzalishaji wa kilimo, kipato na usalama wa chakula. Usalama wa umiliki wa ardhi–kuruhusu upatikanaji, matumizi na udhibiti wa ardhi-, mwishowe huathiri vipato vya jamii na ubora wa maisha[2]. Ardhi pia ni mali muhimu kwa shughuli za biashara na uwekezaji wa ndani/nje, ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa rasilimali, utalii au uzalishaji wa kilimo. Kupata ardhi na usalama wa umiliki wa ardhi vinaathiri maendeleo ya nchi (kiuchumi) kwa ujumla wake.

Nchini Tanzania, ardhi ilianza kuwa mali ya umma baada ya uhuru mnamo mwaka 1961. Sheria ya Ardhi (1999)[3] na Sheria ya Ardhi ya Kijiji (1999)[4] zinatoa **mfumo wa kisheria wa sasa wa haki za ardhi** nchini[5]. Sheria ya Ardhi (1999) inasema kwamba Rais ndiye mwenye dhamana ya kusimamia ardhi yote, kwa niaba ya raia wake. Aina tatu za ardhi zinatambulika hapa: "ardhi ya hifadhi", "ardhi ya jumla" na "ardhi ya kijiji". "Ardhi ya hifadhi" inajumuisha ardhi yote iliyotengwa kwa madhumuni maalum, kama vile uhifadhi wa asili au miundombinu ya umma. "Ardhi ya kijiji" inahusu ardhi yote inayomilikiwa na vijiji vilivyosajiliwa. Ardhi inayobaki inachukuliwa kama "ardhi ya jumla". Tofauti na usimamizi wa serikali kuu kwenye ardhi ya hifadhi na ya jumla, usimamizi wa ardhi ya kijiji uko chini ya serikali za mitaa. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Kijiji (1999), hati miliki zote mbili za ardhi pamoja na haki za kitamaduni zinatambuliwa kisheria kama msingi wa umiliki wa ardhi. Katika maeneo ya vijijini, haki ya ardhi ya kijiji inaweza kutolewa kwa kupitia *'Hati Miliki za Kimila'*, wakati katika maeneo ya mijini *Hati Miliki za Kiserikali* zinaweza kupatikana[6]. Sheria zinaeleza waziwazi ulinzi wa haki sawa kwa wanawake na wanaume linapokuja suala la ardhi. Wakati raia wote wa Kitanzania wana haki sawa ya kumiliki ardhi,

1 Haki za Binadamu, Urasimishaji na Haki za Ardhi kwa Wanawake Kusini na Mashariki mwa Afrika. Benjaminsen, T., Repoti Na. 26, Noragric, Aas Norway; 2005.
2 Uboreshaji wa Utawala katika Sekta ya Ardhi Barani Afrika: Uzoefu wa Tanzania. Kironde J.M.L; 9-10 Machi 2009; http://www.tzdpg.or.tz/fileadmin/_migrated/content_uploads/land_governance_in_Tanzania_paper_by_Kironde.pdf
3 Sheria ya Ardhi (Sura ya113). Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; 1999.
4 Sheria ya Ardhi ya Vijijii (Sura ya 114). Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; 1999.
5 Mifano yote ya sheria ni ya upande wa Tanzania Bara. Sheria ya Zanzibar haijatajwa hapa, kwa kuwa chunguzi kifani zote zilifanyikia upande wa Bara wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
6 Haki ya Umiliki wa Ardhi na Mali. USAID; 2015 https://www.land-links.org/wp-content/uploads/2016/09/USAID_Land_Tenure_Tanzania_Country_Profile.pdf

wageni wanastahili kupata ardhi ya muda tu kwa sababu za uwekezaji kupitia haki za umiliki kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania[7].

**Masuala ya usimamizi wa (rasilimali) ardhi na migogoro ihusuyo haki za ardhi** yamechapishwa sana nchini Tanzania[8]. Mara nyingi migogoro husababishwa na ushindani unaotokana na mahitaji ya ardhi kati ya makundi tofauti ya watumiaji, kama vile wakulima wadogo wadogo dhidi ya makampuni makubwa[9], wafugaji dhidi ya wakulima [10] au wazawa dhidi ya wawekezaji wa utalii. Mfano kwenye hili la mwisho ni Wamasai huko Loliondo (Mkoani Arusha). Huko, Wamasai wameondolewa na kunyimwa ardhi yao ya asili na rasilimali ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambamo wangetumia kwa ajili ya utalii wa uwindaji[11]. Maeneo ya utajiri wa asili nchini Tanzania yanazidi kusimamiwa na kulindwa[12] ili kuhakikisha uhifadhi na kukuza utalii, moja ya nguzo kuu za uchumi wa nchi. Hatua hizi zinahitajika katika kupunguza uharibifu wa rasilimali za ardhi na mazingira unaosababishwa na jamii[13] na shughuli za biashara[14]. Haki ya mazingira yenye afya, ya kutosha kwa afya na ustawi wa watu, inachukuliwa kama sharti la kupatikana kwa haki nyingine za binadamu[15], ikiwa ni pamoja na haki za kuishi, kupata chakula, afya na kiwango cha kutosha cha maisha[16]. Hata hivyo, juhudi za uhifadhi mara nyingi huingiliana na mahitaji ya (rasilimali) ardhi ya jamii zinazozunguka maeneo ya uhifadhi. Mizozo ya ardhi kati ya jamii na mamlaka za uhifadhi hutokea mara kwa mara[17], inaweza kudumu kwa muda mrefu[18] na kuongezeka kwa ukiukwaji wa haki za binadamu kumeripotiwa katika jamii zinazozunguka maeneo kadhaa ya uhifadhi nchini Tanzania[19].

Kukosekana kwa **haki rasmi za ardhi na mipango ya matumizi ya ardhi** katika maeneo mengi ya nchi kunadumisha changamoto zinazohusiana na ardhi. Ili kukabiliana na hili, programu na mipango ya matumizi ya ardhi imeandaliwa ili kuongeza usalama wa umiliki wa ardhi, kwa mafanikio kadhaa[20]. Hata hivyo, haijulikani wazi kama programu hizi zina uwezo na zinafanya kazi kama ilivyokusudiwa kwa ufanisi na kwa muda mrefu katika kushughulikia masuala muhimu yanayohusiana na ardhi, kama vile migogoro ya ardhi, uharibifu wa mazingira, kukosekana kwa usawa wa kijinsia na ukiukwaji wa haki za binadamu.

## CHUNGUZI KIFANI

Tafiti juu ya *"Sauti za Watanzania"* zimegawanyika katika tafiti ndogo ndogo, zilizofanyika kwenye

7 Sheria ya Ardhi (Sura ya113). Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; 1999
8 Serikali yaunda jukumu la kumaliza mizozo ya ardhi. Gazeti la Daily News; 09.11.2018. https://dailynews.co.tz/news/2018-11-095be52b3f8e1dd.aspx
9 K.m.: "Hakuna yoyote": Hadithi Juu ya Ardhi ya Tanzania na Ushirika Mpya wa Ujasiri. African Arguments; 16.05.2018 http://africanarguments.org/2018/05/15/there-isnt-any-tanzanias-land-myth-and-the-brave-new-alliance/
10 E.g.: Viongozi Pwani malizeni mgogoro wa wakulima, wafugaji –Mama Samia. Gazeti la Mwananchi; 29.10.2018
11 Kuipoteza Serengeti. Ardhi ya Wamasai ambayo ilikuwa idumu milele. Taasisi ya Oakland, 2018. https://www.oaklandinstitute.org/sites/oaklandinstitute.org/files/tanzania_maasai_final_web.pdf
12 K.m.: Maeneo ya Uhifadhi Tanzania. Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania -TAWA: https://www.tawa.go.tz/conservation/protected-areas/) or the United Republic of Tanzania's "Environmental Management Act 2004", the "Forest Act 2002" and the "Wildlife Conservation Act 2013".
13 K.m.: Wasiwasi watanda kufuatia shughuli za wanadamu Serengeti, Mara. Gazeti la Daily News; 31.03.2019 https://dailynews.co.tz/news/2019-03-315ca05028b735c.aspx
14 K.m.: Acacia yapigwa faini Sh5.6bn kwa kutiririsha maji yenye sumu. Gazeti la The Citizen; 17.05.2019. https://www.thecitizen.co.tz/News/Acacia-fined-Sh5-6bn-for-leaking-toxic-water/1840340- 5119270-5i5vy7z/index.html
15 Haki za msingi kwa wote duniani, kama zilivyotanabaishwa na kuthibitishwa kwenye Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, Umoja wa Mataifa, 1948. http://www.un.org/en/universal-declaration-human-rights/
16 K.m. Kuhusu haki za binadamu na mazingira. Ofisi ya Kamisheni Kuu ya Haki za Binadamu (OHCHR). https://www.ohchr.org/EN/Issues/Environment/SREnvironment/Pages/AboutHRandEnvironment.aspx
17 JPM aombwa kuingilia kati mgogoro wa Hifadhi ya Kitulo. Gazeti la Mtanzania; 23.04.2019
18 K.m..: Sauti za Watanzania – Utalii na haki za ardhi: uchunguzi kifani wa kijiji kidogo cha Uvinje na Hifadhi ya Taifa ya Saadani. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu; 03.2019. http://ipisresearch.be/publication/voices-tanzania-case-studies-business-human-rights-vol-1/
19 K.m.: Sauti za Watanzania –Uchunguzi kifani juu ya Biashara na Haki za Binadamu, Utafiti wa 5: Uchimbaji wa madini ya chokaa na masuala ya haki za binadamu Mkoa wa Kigoma. E. Mawala (Shirika la IPIS Tanzania); 03.2019. http://ipisresearch.be/publication/voices-tanzania-case-studies-business-human-rights-vol-1/
20 K.m.: Migogoro ya ardhi mkoni Morogoro yashuka. Gazeti la Daily News; 19.02.2019. https://dailynews.co.tz/news/2019-02-195c6babd164302.aspx

maeneo halisi ya kazi, zilizofanywa na asasi za kiraia Tanzania, zenye lengo la kugusa mambo ya msingi juu ya **biashara na haki za binadamu nchini Tanzania**. Kupitia uwepo na shughuli zao za kitafiti, makampuni yanaweza kuwa na mchango mkubwa katika kusimamia na katika kukiuka haki za binadamu. Wakati jukumu la Serikali ni *kuwalinda* raia kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu mahali pa kazi, makampuni yana jukumu la *kuheshimu* haki za binadamu. Hii inamaanisha kwamba lazima yachukue hatua za dhati katika kuzuia ukiukwaji wa haki za binadamu[21].

Tafiti juu ya *"Sauti za Watanzania"* zinahusisha **taarifa mpya za uwandani**, zilizopatikana kwa kupitia k.m. mahojiano na wadau, ushuhudiaji au hojaji, pamoja na vyanzo vya data za upili kama vile mifumo ya sheria za ndani (na za kimataifa), ripoti zilizochapishwa au nyaraka (sera) za makampuni. Chambuzi za sasa zinatoa taarifa ambazo hazikuchapishwa awali, zinatoa picha mpya na kuruhusu kuweka **mapendekezo ya wazi** kwa wadau mbalimbali wanaohusika.

Toleo la pili la *"Sauti za Watanzania"* linaeleza **tafiti nne kifani zinazojikita kwenye "haki za ardhi na mazingira"**. Tafiti hizi zinazungumzia masuala mawili muhimu hapa: (1) ni kwa namna gani hatua kwa ajili ya kuongeza **usalama wa umiliki wa ardhi na mipango ya matumizi ya ardhi** inaathiri jamii ziishizo vijijini, na (2) ni kwa jinsi gani **juhudi za uhifadhi** zinaathiri ardhi na haki za binadamu kwenye vijiji vilivyo karibu na maeneo ya uhifadhi?




*Dokezo la tafiti zilizomo kwenye chapisho la "Sauti za Watanzania –chunguzi kifani juu ya Biashara na Haki za Binadamu (Toleo la 2)"*

21 Soma zaidi kwenye k.m.: Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu: Utekelezaji Mfumo wa 'Kulinda, Kuheshimu na Kupata Unafuu wa Kisheria' wa Umoja wa Mataifa, Ofisi ya Kamisheni Kuu ya Haki za Binadamu (OHCHR), 2011. https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciplesBusinessHR_EN.pdf.


**Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT)** ilifanya utafiti juu ya athari za haraka za Programu ya Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi kwa jamii ziishizo wilayani Kilombero (Morogoro). Programu ya Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi ni mpango mkubwa zaidi wa umilikishaji wa ardhi hadi leo nchini Tanzania, unaolenga kuboresha usalama wa umiliki wa ardhi (yaani upatikanaji salama, matumizi na udhibiti wa ardhi) kupitia urasimishaji wa umiliki bora wa ardhi. Ulifanyika kati ya mwaka 2016-2019 Morogoro, mkoa "maarufu" kwa migogoro yake mingi ya ardhi.

**HakiArdhi (Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Masuala ya Ardhi**) ililenga jinsi mpango wa matumizi bora ya ardhi unaweza kuwa nyenzo ya kukuza usimamizi wa ardhi, kama inavyoonekana kwenye uchunguzi kifani wa Wilaya ya Kilolo, Iringa. Mpango wa kijiji wa matumizi bora ya ardhi hutenga eneo la ardhi ya kijiji na kuwezesha uwekaji mipaka wa maeneo ya ardhi. Pia unajadili na kuamua juu ya matumizi na umiliki wa ardhi hii. Sera za mpango ya matumizi bora ya ardhi nchini Tanzania zilitungwa kufuatia mzozo unaokua unaohusu ardhi na maliasili na hitaji la usalama ulioboreshwa wa umiliki wa ardhi.

**Asasi ya TAWEA** imechunguza jinsi maeneo ya uhifadhi mkoani Kigoma yanaweza kusababisha masuala ya ardhi na haki za binadamu katika jamii zinazoishi karibu na maeneo kama haya. Utafiti ulilfanyika kwenye vijiji 2 wilayani Kasulu, vilivyo karibu na maeneo ya uhifadhi ya Hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini na Pori la Akiba la Moyowosi. Ukuaji wa idadi ya watu na hitaji kubwa la ardhi zaidi kwa ajili ya kilimo na rasilimali katika kuboresha maisha ya wanakijiji unazidi kuchochea matumizi makubwa ya rasilimali zinazopatikana ndani ya vijiji hivi. Hatima yake ni kwamba, shughuli za wanakijiji zimeongezeka katika hifadhi za karibu, kitu ambacho ni ukiukwaji wa sera za serikali za uhifadhi kwa ajili ya maeneo haya.

**Asasi ya CEDESOTA** ilifanya utafiti kuona jinsi ukaribu wa Hifadhi ya Taifa ya Arusha (wilayani Arumeru, Arusha) unavyoathiri haki za binadamu katika vijiji vilivyo karibu na hifadhi hiyo. Huko, migogoro kati ya wanyamapori na binadamu inaongezeka, kadri idadi ya watu pamoja na rasilimali mchanganyiko zilizopo inasababisha kuongezeka kwa mwingiliano kati ya wanyamapori na jamii za karibu. Kadri mwingiliano huu mara nyingi unaathiri vibaya uendelevu wa binadamu na wanyamapori, ndivyo unavyozidi kuwa tishio kwa haki za msingi za jamii na uhifadhi wa wanyamapori.

**UTAFITI WA 1:**




## Athari za haraka za Programu ya Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi kwa Jamii ziishizo Wilaya ya Kilombero, Mkoa wa Morogoro *(Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira)*

*Ardhi ni muhimu kwa maendeleo ya jamii zote. Nchini Tanzania, zaidi ya asilimia 65 ya wananchi wanapata riziki kupitia shughuli zinazohusiana na ardhi, haswa kilimo. Katika mazingira ya vijijini, umuhimu wa ardhi ni mkubwa zaidi kwani ardhi katika maeneo ya vijijini hutoa fursa ya ufikiaji wa rasilimali muhimu kwa usalama wa jamii.*

Hata hivyo, matumizi tofauti/anuwai ya ardhi yamesababisha migogoro ambayo kwa nyakati tofauti imesababisha vifo, majeraha, na kupotea kwa mali. Kuongezeka kwa idadi ya watu, uwekezaji na ubinafsi katika umiliki wa ardhi nchini Tanzania kumesababisha migogoro mingi ambayo imedai hatua kubwa zenye kulenga kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi. Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi (LTSP), ambayo ni msingi wa ripoti hii, ni moja ya programu hizo.

Ripoti hii fupi imejikita kuonesha athari za haraka za Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi iliyotekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wilayani Kilombero, mkoa wa Morogoro. Tafiti hii mahususi kwa wilaya ya Kilombero, haswa, ilikuwa muhimu kwani wilaya inatoa fursa za kipekee za kiuchumi na za kimazingira kwa uwekezaji katika ardhi, fursa za uchumi wa ndani na faida za mazingira. Vile vile, Wilaya ya Kilombero iko jirani na wilaya za Mvomero na Kilosa, ambapo mizozo ya wafugaji imeripotiwa mara kwa mara.

Utafiti ulijikita kuchambua athari za haraka hususani katika maeneo ya biashara, haki za binadamu na mazingira zilizotokana na utekelezaji wa program ya Uwezeshaji Umilikishaji Ardhi iliyoanza mwaka 2016 na kumalizika 2019.

Ripoti imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza, ambayo ni utangulizi wa ripoti inatoa ufahamu juu ya msingi wa tafiti. Inazungumza kwa ufupi masuala muhimu ya usimamizi wa ardhi wilayani Kilombero na Tanzania kwa jumla, na inaelezea programu ya LTSP na eneo la tafiti. Kwa kuongezea, utangulizi umetoa maelezo juu ya umuhimu wa utafiti na malengo. Sehemu ya pili ya utafiti inaonyesha njia iliyotumika kufanya utafiti. Sehemu ya tatu imejikita kueleza matokeo makuu ya utafiti. Uchambuzi wa matokeo umefanywa kwa kuakisi athari za biashara, haki za binadamu na mazingira zilizotokana na programu ya LTSP. Athari chanya na hasi zilipatikana. Athari chanya zilijumuisha kuongezeka maeneo ya vijiji yaliyopimwa, uanzishwaji wa vituo vya udhibiti wa kijiografia, ugawaji wa vyeti vya ardhi vya vijiji, uundaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya, maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kuongezeka kwa usalama wa umiliki wa ardhi. Athari hasi zilizobainishwa ni upoteaji wa ardhi na haki ya umiliki wa ardhi, udhibiti duni wa ardhi na ardhi haba kupangwa kwa wafugaji. Tathmini ya athari za haraka za programu inahitajika sana ili kunakili shughuli za programu ya LTSP katika mikoa mingine ya nchi. Sehemu ya nne ya utafiti imeanisha hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

Kwa ujumla, utafiti unatambua kazi iliyofanywa na programu ya LTSP katika mkoa wa Kilombero. Aidha, utafiti unasifu ubia wa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali ulioruhusu Asasi za kiraia, hususani Jumuiko la Ardhi Tanzania (TALA), kufanya uchechemuzi sambamba na utekelezaji wa programu. Kwa kutambua changamoto za utekelezaji wa programu, utafiti pia umetoa mapendekezo ya kuboresha zaidi usimamizi wa ardhi katika maeneo mengine ya nchi.

**UTAFITI WA 2:**




## Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kama Nyenzo ya Kukuza Usimamizi wa Ardhi: Uchunguzi kifani wa Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa *(Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Masuala ya Ardhi)*

*Ardhi ni rasilimali ya msingi kwa jamii kwa ajili chakula, maji, nishati, mavazi na malazi. Ili kukabiliana na uhaba wa rasilimali ardhi na kuongezeka kwa migogoro juu ya utumiaji wa ardhi, jukumu la upangaji wa matumizi ya ardhi kwa usimamizi endelevu wa ardhi na maliasili ni muhimu. Tafiti mbalimbali zimefafanua kwa kina umuhimu wa mipango ya matumizi ya ardhi katika kushughulikia changamoto za haki za ardhi endapo mipango hii itaandaliwa kwa njia shirikishi na kukamilisha hatua zote kwa mujibu wa sheria na miongozo. Hii ni changamoto katika muktadha wa Tanzania kutokana na kasi ndogo ya kuandaa mipango hii nchi nzima.*

Kuna dhana kuwa maamuzi yasiyoridhisha katika usimamizi na matumizi ya ardhi yanatokana na kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi. Mfano wa maamuzi hayo ni pamoja na, ugawaji wa ardhi kubwa kwa wawekezaji bila ya ridhaa ya wanavijiji, migogoro ya ardhi baina ya watumiaji tofauti wa ardhi kama vile wakulima na wafugaji, au wawekezaji na wanavijiji, migogoro ya mipaka baina ya vijiji, na shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, uchomaji wa mkaa, uvunaji wa miti na shughuli zingine za wanadamu kwenye maeneo yaliyotengwa kama hifadhi ya misitu, vyanzo vya maji na maeneo ya mito. Uandaaji wa mipango ya matumzi ya ardhi kuwa shirikishi inahusianishwa na mipango iliyoboreshwa ya kutatua matatizo ya ardhi, mazingira, madhara ya mabadiliko ya tabia nchi, ukiukwaji wa haki za binadamu na usawa wa kibinadamu.

Katika utafiti huu, matokeo yamewasilishwa juu ya mchakato wa upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji na mchango wake katika kukuza na kuimarisha usimamizi wa ardhi na mali asili. Utafiti umekusanya matokeo ya upangaji na utekelezaji wa matumizi ya ardhi kutoka vijiji vya Kihesamgagao na Lyamko wilayani Kilolo

katika Mkoa wa Iringa kuhusiana na utawala wa ardhi ya vijiji, migogoro ya ardhi, uwekezaji, usimamizi wa mazingira na haki za wanawake katika ardhi.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa mipango ya matumizi ya ardhi ina mahusiano na masuala yaliyotajwa hapo juu kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, juu ya usimamizi wa ardhi ya vijiji, mipango ya matumizi ya ardhi inatengeneza nafasi ya ufanyaji wa maamuzi kidemokrasia kwa kila mwanakijiji kushiriki katika kutoa maoni na kufanya maamuzi yanayohusisha vikundi vyote vya kijamii. Halikadhalika, mipango ya matumizi ya ardhi inaweza kupunguza migogoro ya ardhi pale kunapokuwepo ushirikishwaji dhabiti wa jamii katika kuamua matumizi ya ardhi ya kijiji. Utafiti ulibaini pia kuwa kuwa mipango ya matumizi ya ardhi ina nafasi katika kutatua migogoro ya mipaka baina ya vijiji vinavyopakana.

Kuhusu utunzaji wa mazingira, imebainishwa na utafiti kuwa mipango ya matumizi ya ardhi inatoa fursa kwa wanakijiji kupanga matumizi ya ardhi yao sambamba na ulinzi wa rasilimali nyingine kama vile vyanzo vya maji na misitu. Halikadhalika, kwa upande wa haki za ardhi kwa wanawake, mipango ya matumizi ya ardhi hutoa fursa kwa wanawake kushiriki katika maamuzi juu ya ardhi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Ardhi namba 4 ya 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya 1999 na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi namba 6 ya 2007 ambayo inasisitiza ushiriki wa wanawake katika kila hatua ya mchakato ikiwa ni pamoja na kuwa na wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji na kupewa vyeti vya hakimiliki ya kimila.

Kwa upande mwingine mipango ya matumizi ya ardhi ina athari kwa wazalishaji wadogo katika usimamizi, na ugawaji wa ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi na utunzaji wa mazingira. Kwa mfano, bajeti finyu inayopangwa na serikali kwenye uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi hutoa mwanya kwa wawekezaji na asasi za kiraia kufadhili mipango hii ambapo athari yake kwa maslahi ya wazalishaji wadogo kutokupewa kipaumbele katika mchakato mzima.

Pamoja na ukweli kuwa mipango ya matumizi ya ardhi inaweza kuwa na mchango katika utunzaji wa mazingira na rasilimali zake, wakati mwingine mikakati hii imekuwa haizingatii mahitaji ya wazalishaji wadogo ambao kwa miaka yote wamekuwa wakitumia ardhi husika kwa ajili ya kuendesha maisha yao.

Ilibainika pia kuwa kuna ushirikishwaji hafifu wa wanawake katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye kutokana kuaminika kuwa ni wanaume tu ndio wenye kufahamu habari za kijiji kwa ufasaha na uhakika zaidi kuliko wanawake, jambo ambalo hata hivyo wanawake walilipinga sana kwa hoja ya kuwa hata wao wana uelewa kuhusiana na vijiji vyao.

Kwa ujumla, pamoja na faida za mipango ya matumizi ya ardhi zilizobainishwa ni ngumu kuhitimisha kuwa faida hizi zinaweza kujitokeza ghafla kutokana na uwepo wa mipango hii. Kuna changamoto kadha wa kadha ambazo zimebainishwa kwenye mchakato wenyewe ambazo zinafifisha ubora wa mipango ya matumizi ya ardhi katika kufikia malengo yake hususani kwa wazalishaji wadogo wa ardhi ambao ndio watumiaji wakubwa wa ardhi za vijiji.

Mapendekezo ya utafiti huu ni pamoja na kuboresha mchakato wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa lengo la wazalishaji wadogo kushiriki kikamilifu. Endapo wanavijiji watakuwa na uamuzi wa mwisho katika mipango ya matumizi ya ardhi basi mipango hii itatekelezwa na kudumu kwa muda mrefu zaidi. Vile vile, mfumo wa kisheria unatakiwa kuelekeza kwa uwazi kabisa kuwa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kiwe ndio kigezo mahsusi katika ugawaji wa ardhi ya kijiji kwa wawekezaji.

Serikali isiidhinishe ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji kwenye ardhi za vijiji pasipo mipango ya matumizi ya ardhi kukamilika. Hii ni kwa sababu uwekezaji wowote utakaotanguliwa na mipango ya matumizi ya ardhi utawapa fursa wanavijiji kuamua kama wanayo ardhi ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji au ni kwajili ya matumizi yao tu. Pamoja na hayo kuna umuhimu wa kutambua na kuheshimu maarifa ya asili ya wanavijiji katika kutunza na kuhifadhi mazingira. Hii itawezekana kwa kuwashirikisha wakulima na

wafugaji katika utungaji wa Sera na Sheria kwasababu wanayo mengi ya kuchangia kutokana na historia waliyonayo katika matumizi ya ardhi ambayo yanaweza kuboresha Sera na Sheria wakati zikizingatia mahitaji ya kijamii na kiuchumi kwa wazalishaji wadogo. Mwisho, inapendekezwa kuwa haki za ardhi kwa wanawake zisitafsirike tu kuwa zinaweza kupatikana kwa kuwapatia wanawake vyeti vya hakimiliki ya kimila bali haki hizi zitambulike kwa upana wake kwa kuhakikisha kuwa jamii inafahamu haki hizi kwa undani zaidi.

**UTAFITI WA 3**



## Masuala ya Ardhi na Haki za Binadamu baina ya Jamii ziishizo karibu na maeneo ya uhifadhi mkoani Kigoma: Uchunguzi kifani wa vijiji vya Kagera Nkanda na Mvinza karibu na Pori la Akiba la Moyowosi na Hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini *(Asasi ya TAWEA)*

Madhumuni ya ripoti hii ya Utafiti ni kuweka bayana changamoto za masuala ya ardhi na haki za binadamu kwa jamii ambazo zinapakana na maeneo yaliyohifadhiwa katika vijiji vya Kagera-Nkanda na Mvinza vinavyopakana na Msitu wa Hifadhi wa Makere Kusini na Pori la Akiba la Moyowosi katika mkoa wa Kigoma. Wanavijiji katika vijiji hivi wanategemea kilimo, ufugaji wa wanyama, uvuvi na ufugaji wa nyuki ili kuendesha maisha yao. Ongezeko la idadi ya watu na pamoja na mahitaji ya ardhi ya ziada kwa ajili ya kilimo na rasilimali muhumu za maisha yanaongeza shinikizo kwa maliasili zinazopatikana katika maeneo yaliyohifadhiwa na kuwafanya baadhi ya wakazi wa vijiji hivyo kufanya shughuli za kiuchumi ndani ya mipaka ya maeneo yaliyohifadhiwa.

Hali hii inazidisha utata baina ya wanavijiji na mamlaka za uhifadhi ambazo zina majukumu ya kusimamia sheria na kanuni za kulinda maeneo yaliyohifadhiwa.

Lengo la utafiti huu ni kubaini masuala ya ardhi na haki za binadamu yanayohusiana na wakazi wa vijiji vya Kagera-Nkanda na Mvinza (Kigoma). Maswali ya msingi ya utafiti huu ni; (1) Ni migogoro ipi ya matumizi ya ardhi iliyopo katika vijiji vinavyopakana na Msitu wa Hifadhi wa Makere Kusini na Pori la Akiba la Moyowosi? (2) Nini athari za migogoro ya ardhi kwa vijiji vinavyopakana na Msitu wa Hifadhi wa Makere Kusini na Pori la Akiba la Moyowosi? (3) Nini faida ya uhifadhi shirikishi katika kutatua masuala ya migogoro ya ardhi baina ya vijiji na Msitu wa Hifadhi wa Makere Kusini na Pori la Akiba la Moyowosi?.

Taarifa hii inatokana na ukusanyaji wa taarifa za awali na ziada kutoka kwa wananchi na mamlaka za uhifadhi kutokana na usaili wa kutumia madodoso, majadiliano na ziara (kutembelea) maeneo ya utafiti katika vijiji husika katika kipindi cha mwezi Agosti na Septemba,2019.

Matokeo ya utafiti huu yanabainishwa katika makundi makuu matatu; (1) Uwepo wa migogoro ya ardhi na ukiukwaji wa haki za binadamu katika vijiji vya Kagera-Nkanda na Mvinza kutokana na shughuli za kibinadamu ndani ya maeneo ya hifadhi kinyume na sheria za uhifadhi. Matumizi ya nguvu kupita kiasi katika utekelezai wa sheria kama vipigo na kutaifisha mali za wanavijiji na hivyo matendo haya kuonekana kwamba ni ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na mamlaka za uhifadhi katika maeneo hayo. (2) Uwepo wa migogoro ambayo haijatatuliwa kutokana na ukosefu wa taarifa sahihi na ushirikwishaji hafifu wa wananchi juu ya mipango ya matumizi ya ardhi, uhakiki wa ardhi na uwekezaji wa kitalii unaohusisha serikali na sekta Binafsi. (3) Uwepo wa miradi ya uhifadhi shirikishi kama ufugaji wa nyuki na elimu ya uhifadhi wa mazingira inayochangia kuinua hali ya maisha ya wanavijiji wanaopakana na maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kuongeza ushiriki wao katika ulinzi wa rasilimali zinazopatikana katika msitu wa hifadhi na pori la akiba.

Mapendekezo kutokana na utafiti huu:

- Jitihada zaidi za uhifadhi shirikishi zinahitajika kuanzishwa na kuendelezwa kitu ambacho kitaongeza uelewa kwa wananchi juu ya masuala ya uhifadhi na umiliki wa rasilimali misitu. Jitihada hizi zitatoa fursa za Kuongeza kipato mbadala na hivyo kuboresha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa maeneo ya misitu na wanyama pori yanayopakana na vijiji vyao.
- Wadau kwa ngazi tofauti washirikishwe katika uwekaji wa mipaka na kuboresha matumizi bora ya ardhi kwa njia shirikishi. Hii itasaidia kupunguza migogoro ya mipaka ya ardhi baina ya vijiji na maeneo yaliyohifadhiwa pamoja na kuwasaidia wananchi hao kufaidika na ardhi iliyopo katika vijiji vyao ambayo inamilikiwa na wananchi wageni kutoka maeneo mengine.
- Ufafanuzi wa uhakiki wa mipaka uliofanyika mwaka 2007 unahitajika ili kuondoa migogoro ya mipaka inayoendelea katika kijiji cha Mvinza kutokana na uwekaji wa alama mpya za mipaka zenye utata baina ya Kijiji na maeneo yaliyohifadhiwa.
- Jitihada za kutoa Elimu zaidi ziongezwe hasa juu ya haki na wajibu wa wadau mbali mbali katika uhifadhi. Maaofisa wa uhifadhi wapewe elimu ya kutosha ili katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kutumia sheria ya misitu na wanyama pori wasikiuke haki za kimsingi za binadamu. Aidha, wananchi wafahamu wajibu wao wa uhifadhi kama inavyoelekezwa na sheria za Tanzania.

**UTAFITI WA 4:**




## Athari za Hifadhi ya Taifa ya Arusha kwa Haki za Binadamu katika Vijiji vya Olkung'wado na Ilkirimuni – Wilaya ya Arumeru, Arusha *(Asasi ya CEDESOTA)*

*Mgogoro wa Wanyamapori na Binadamu umekuwa tatizo kubwa katika maeneo mengi ya Tanzania, sio tu wilayani Arumeru (Mkoa wa Arusha). Ongezeko la idadi ya watu pamoja na upatikanaji wa rasilimali mara nyingi ndio sababu ya kuongezeka kwa mwingiliano kati ya wanyamapori na jamii. Kwa jamii inayoishi karibu na maeneo yaliyohifadhiwa, hali hiyo hujitokeza sana.*

CEDESOTA, kwa msaada wa shirika la IPIS, ilifanya utafiti mdogo ili kujua sababu na athari za mgogoro wa wanyamapori na binadamu katika vijiji vya Olkung'wado na Ilkirimuni vilivyoko Wilayani Arumeru na ambavyo hupakana na Hifadhi ya Taifa ya Wanyamapori ya Arusha (Mkoa wa Arusha, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania). Kusudi la utafiti huu lilikuwa kubaini athari zinazotokana na Hifadhi ya Kitaifa ya Arusha kwa haki za binadamu na haki za ardhi katika vijiji vya Olkung'wado na Ilkirimuni. Utafiti huo ulifanywa kwa kutumia mahojiano yaliyoandaliwa na shirika la CEDESOTA kwa mamlaka za husika za Wilaya Kata na vijiji pamoja na wadau mhimu. Takwimu zilikusanywa katika vijiji vya Olkung'wado na Ilkirimuni na kuchambuliwa kwakuhusianisha na migogoro ya Wanadamu na Wanyamapori, masuala ya ardhi, uhusiano kati ya jamii na mamlaka ya uhifadhi na faida jamii inayopata kwa kuwa jirani na Hifadhi ya Kitaifa ya wanyamapori Arusha. Mwingiliano kati ya jamii na wanyamapori katika vijiji viwili vilivyotajwa haujasababisha mauaji wala majeruhi katika jamii japo inatokea kwa kiwango kidogo kwa mifugo. Tembo walitajwa kuharibu mazao, haswa kwa kipindi cha mwaka 2018/19 na kusababisha uhaba wa chakula na hivyo kuhatarisha haki ya chakula na maisha kwa jamii zilizopo karibu na Hifadhi ya Taifa ya Wanyamapori ya Arusha. Wanajamii wanaona mwingiliano huo kama tishio la maisha yao na tarrifa zinazopelekwa Halmashauri za Vijiji husika na hatimaye halmashauri ya Wilaya mara nyingi hubaki bila suluhisho la kudumu. Fidia iliyowekwa kisheria pia ni ndogo sana haitoshi kulipia hasara halisi inayotokea.

Migogoro ya ardhi kati ya vijiji haipo isipokuwa kwa vijiji vilivyopakana na mbuga ya hifadhi, kati ya vijiji vyenyewe na mamlaka ya uhifadhi. Mahusiano kati ya jamii na mamlaka ya uhifadhi ni mgumu kwa kutokuwa na mawasiliano kidogo na pia kufanya maamuzi yasio shirikishi juu ya uhifadhi na mahitaji mengine, mara nyingi hali hii haiwaridhishi wanajamii.

Pamoja na changamoto hizi, jamii hupata faida mbalimbali kutokana na Hifadhi ya Taifa ya Arusha, ikiwemo mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi 30 vya wanawake, fursa za masoko kama kuuza bidhaa zao kwa watalii, hifadhi ya Taifa Arusha huchangia gharama za ujenzi wa vyumba vya madarasa na zahanati kwa asilimia 70 na kutoa ajira kwa vijana wenye tasnia ya utalii.

1. Kwa kuhitimisha inaonyesha kuwa migogoro ya wanyamapori na wanadamu huleta changamoto kubwa kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi za wanyamapori. Migogoro hii ni mapungufu makubwa kuhusu uhifadhi shirikishi. Kuhusisha jamii katika mchakato wa utawala na usimamizi ni muhimu kwa uhifadhi endelevu na inatoa motisha kwa jamii kusaidia katika uhifadhi na ulinzi kwa wanyamapori.

2. Ili kuhakikisha ushiriki mzuri wa jamii katika uhifdhi wa wanyamapori, inapendekezwa kufanya mapitio ya viwango vya fidia katika sheria namba 5 ya wanyamapori ya mwaka 2009 ili kutoa fidia halisi ya hasara zinazopatikana kutokana na mwingiliano wa wanadamu na wanyama wa pori; kujenga uelewa zaidi wa jamii juu ya haki na majukumu yao katika uhifadhi na wajue utaratibu wa kufuatilia na kupata fidia inapotokea uharibifu wa mazao na mali zao; kuweka mifumo rahisi ya mawasiliano kati ya jamii na mamlaka za uhifadhi na upatikanaji taarifa kwa jamii, kuhakikisha wote wanashiriki katika uhifadhi na michakato ya kufanya maamuzi. Kuweka mradi wa ufugaji nyuki hasa katika eneo linalotenganisha mbuga na vijiji kama chanzo mbadala cha mapato ya jamii na pia nyuki husaidia kulinda msitu na kuzuia tembo kutoka maeneo yaliyohifadhiwa kuja kwenye mashamba ya mazao ya wananchi.

## HITIMISHO JUMUISHI NA MAPENDEKEZO

Chunguzi kifani nne zilizoelezewa kwenye toleo hili la pili la "*Sauti za Watanzania*" zinalenga mambo mawili ya msingi ndani ya mada kuu ya **"haki za ardhi na mazingira"**: 1) ni kwa namna gani hatua za kuongeza **usalama wa umiliki wa ardhi na mipango ya matumizi ya ardhi** zinaathiri jamii ziishizo vijijini, na (2) ni kwa jinsi gani **juhudi za uhifadhi** zinaathiri ardhi na haki za binadamu katika vijiji vilivyo karibu na maeneo ya uhifadhi?

Pamoja na kuwa tofauti katika muktadha na mada zao mahususi - kuanzia Programu ya Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi Wilayani Kilombero (Morogoro), hadi Mpango wa kijiji wa matumizi bora ya ardhi wilayani Kilolo (Iringa) na maeneo ya uhifadhi mikoa ya Kigoma na Arusha – tafiti zote nne zinasisitiza umuhimu wa ardhi kwa maendeleo ya jamii na utendaji wa haki. **Kutafuta fursa za maisha** (na rasilimali zinazohusiana na ardhi) kunazingatia masuala mengi ya ardhi yaliyogunduliwa kwenye tafiti hizi. Ndio maana watu wanatumia maeneo ya uhifadhi kiharamu kama chanzo cha rasilimali (Hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini, Pori la Akiba la Moyowosi (Kigoma)) au kwanini kuna ugomvi juu ya mipaka ya ardhi (kijiji cha Mvinza (Kigoma); kijiji cha Olkung'wado (Arusha). Ndio maana watu wanapora ardhi ya wengine (vijiji vya Kihesa Mgagao na Lyamko (Iringa)), kwanini makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi yanagombana kutokana na umiliki wa ardhi (Hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini (Kigoma); vijiji vya Miwangani, Sagamaganga na Mpanga Kisawasawa (Morogoro); vijiji vya Kihesa Mgagao na Lyamko (Iringa); kijiji cha Olkung'wado (Arusha) na kwanini migogoro inayotokana na kuvamia maeneo ya uhifadhi inaweza kusababisha ongezeka la ukiukwaji wa haki za binadamu wakati wa utekelezaji wa sheria za uhifadhi, kama vile kutiwa nguvuni, kufungwa jela, kupigwa, kutozwa faini kinyume na sheria na kupora mali za wanakijiji (Hifadhi ya Msitu wa Makere Kusini (Kigoma)).

Kimsingi, masuala haya yanatokana na kukosekana kwa uwazi na usalama wa umiliki wa ardhi. Hivyo basi, **Mpango shirikishi wa matumizi bora ya ardhi na umilikishaji wa ardhi**, kuhakikisha **umiliki salama wa ardhi**, vinachukuliwa kuwa muhimu katika kutatua masuala ya ardhi na kulinda na kukuza haki za watumiaji mbalimbali wa ardhi. Inapotekelezwa, michakato hii inaonekana kuleta **athari chanya**, ikiwa ni pamoja na ongezeko la utoaji wa hati miliki za ardhi – ikiwa ni pamoja na kwa wanawake pia -, uhifadhi jamii na michakato ya kidemokrasia zaidi katika kufanya maamuzi juu ya ardhi, kama inavyoonekana

katika chunguzi kifani za wilaya za Kilolo na Kilombero. Yasipokuwepo haya, ugomvi juu ya upatikanaji wa ardhi, umiliki na utumiaji wa ardhi unaweza kuzidi. Haya yanaweza kuchochea migogoro ya muda mrefu na kukuza masuala ya haki za binadamu, kama invyoonekana kwenye chunguzi kifani za Mkoa wa Kigoma. Licha ya uwepo wa mipango tofauti ya matumizi ya ardhi na programu za haki za ardhi, umilikishaji wa ardhi na usimamizi sahihi wa ardhi bado hautoshi sehemu kubwa ya nchi. Kama inavyoonekana kwenye Mipango ya kijiji ya matumizi bora ya ardhi na Programu ya Kuwezesha Umilikishaji wa Ardhi, **michakato mara nyingi haikamiliki au kuwa sawia**, kutokana na, pamoja na mambo mengine, ukwasi, uwezo mdogo wa wadau, ufahamu mdogo na kukosekana kwa vitendo shirikishi vya dhati. Mapungufu haya yana athari kubwa. Kubagua makundi fulani ya wadau, kama wafugaji, kwenye michakato ya usimamizi wa ardhi kulionekana kusababisha migogoro endelevu ya ardhi katika wilaya ya Kilombero (kijiji cha Sagamaganga). Kukosa kuandaa mipango kamili ya matumizi ya ardhi ya vijiji - yaani kushindwa kutekeleza mchakato huo kupitia hatua zote zinazohitajika -, kunawaacha bila mpango thabiti wa matumizi halisi ya ardhi iliyotengwa, na kusababisha migogoro na mijadala (vijiji vya Kihesa Mgagao na Lyamko, Wilaya ya Kilolo). Hata katika mchakato shirikishi, kukosekana kwa taarifa za kutosha na ufahamu mara nyingi husababisha maamuzi ambayo huleta minong'ono baadaye, pale matokeo yote yanapoonekana. Hii inaonekana hasa wakati ardhi ya kijiji inapokuwa imetengwa kwa ajili ya uwekezaji.

**Mawasiliano na mwamko mdogo** juu ya haki, kanuni na maamuzi huongeza mizozo na migogoro inayohusiana na ardhi. Kwa mfano, mawasiliano duni yanayohusu mipaka ya ardhi ya vijiji na uwekezaji wa kitalii yamesababisha mzozo wa muda mrefu juu ya umiliki wa ardhi kati ya kijiji cha Mvinza na mamlaka za uhifadhi mkoani Kigoma. Uhamasishaji mdogo juu ya taratibu za kutatua mgongano kati ya wanyamapori na binadamu na utoaji fidia, kwa upande mwingine, unawaacha wanakijiji waishio karibu na Hifadhi ya Taifa ya Arusha (vijiji vya Olkung'wado na Ilkirimuni) wakiwa na hasira na kuzinyooshea kidole mamlaka za vijiji na Hifadhi kwa kuthamini uhifadhi wa wanyamapori kuliko maisha ya binadamu na mambo yao. Pamoja na mipango madhubuti ya matumizi bora ya ardhi, kuna umuhimu wa kuongeza uhamasishaji juu ya udhibiti wa mazingira na uhifadhi pamoja na kupashana habari juu ya haki na majukumu ya wadau mbali mbali katika uhifadhi, hasa katika maeneo yaliyo kwenye ardhi ya hifadhi. Kwa mantiki hiyo, uhifadhi wa mazingira unaweza kuboreshwa, wakati migogoro inayohusiana na ardhi na rasilimali inaweza kupungua. Kuanzisha na kutekeleza **programu za uhifadhi jamii** kunaweza kuwa njia mojawapo ya kuongeza ushiriki wa jamii katika uhifadhi wa maeneo ya uhifadhi na rasilimali zao wakati mahitaji ya maisha ya watu katika maeneo haya yakizingatiwa.

**Mapendekezo** kupitia toleo hili la tafiti kuhusu *"Sauti za Watanzania"* ni pamoja na:

- **Umilikishaji wa ardhi na michakato ya mipango ya matumizi ya ardhi vinatakiwa kutekelezwa kikamilifu** nchini kote. Ni nyenzo muhimu za kutatua matatizo ya masuala yanayohusiana na ardhi na kulinda na kukuza haki za watumiaji tofauti wa ardhi.
- **Michakato** ya usimamizi wa ardhi **inatakiwa kuwa shirikishi na jumuishi kabisa** ili waweze kupata mafanikio ya kudumu juu ya usalama wa haki na kuzuia mizozo. Mahusiano yasiyo na usawa na kutowahusisha wadau katika michakato hii ni vema viepukwe ili kuhakikisha matokeo chanya.
- **Michakato** ya mipango ya matumizi ya ardhi **inatakiwa kurahisishwa** ili kuhakikisha wanakijiji wanashiriki kikamilifu na jamii inapata umiliki endelevu na sio (tu) na viongozi wa vijiji au wadau wa nje, kama ambavyo mara nyingi imekuwa iikishuhudiwa.
- **Kujengewa uwezo na kuhamasishana katika ngazi za mitaa kunatakiwa kuimarishwa** – ikiwa ni pamoja na wanajamii, serikali za mitaa, mamlaka na taasisi za ardhi – ili kila mtu atekeleze majukumu yake kwa ufanisi katika michakato ya umilikishaji wa ardhi, uwekaji mipango ya matumizi ya ardhi na uhifadhi.
- **Mipango ya uhifadhi jamii inatakiwa kuendelezwa na kuungwa mkono**, ili kuongeza uhamasishaji wa ndani na umiliki wa uhifadhi, wakati fursa mbadala za maisha kwa jamii ziishizo vijijini zikitolewa. Kutambua mchango wa maarifa ya jamii ziishizo vijijini katika uhifadhi wa mazingira kungesaidia zaidi kutokomeza visababishi vya migogoro.

- **Mawasiliano kati ya jamii na mamlaka za uhifadhi yanatakiwa kuboreshwa na kurahisishwa.** Njia za sasa za mawasiliano mara nyingi ni za urasimu na zenye kuhusisha wakubwa kwanza kabla ya walio chini kimamlaka, na hazishirikishi jamii kwenye michakato ya kufanya maamuzi au utoaji habari kikamilifu.

- **Programu za umilikishaji /mipango ya ardhi zinatakiwa kwenda zaidi ya kutoa hati miliki za ardhi.** Kuhakikisha haki za ardhi kwa wote, ikiwa ni pamoja na zile zinazowahusu wanawake na makundi mengine yaishiyo katika mazingira magumu, kunahitaji mabadiliko ya msingi ya kijamii ambayo ni zaidi ya utoaji wa Hati Miliki za Kimila. Hii ni pamoja na kukuza usawa wa kijinsia, uhamasishaji na uwezeshaji wa makundi yote ya wenye kuhitaji haki

- **Rasilimali za kutosha zinatakiwa kutengwa** kwa ajili ya utekelezaji kamili wa mipango, kama vile mipango ya vijiji ya matumizi bora ya ardhi, utoaji wa hati miliki za ardhi au uungaji mkono wa mipango ya uhifadhi jamii.

Project funded by the EUROPEAN UNION

"Sauti za Watanzania" ni ushirikiano baina ya asasi za kiraia za Tanzania, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Asasi ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania (BHRT) na Shirika la IPIS. Chapisho hili ni sehemu ya mradi wa '**Uboreshaji wa ufuatiliaji, tafiti na majadiliano juu ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania**' unaotekelezwa na CHRAGG, BHRT na IPIS, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya, Kitengo kinachoshughulikia Demokrasia na Haki za Binadamu (EIDHR).

Mawasiliano: bizhumanrightsTanzania@gmail.com